

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



Tarehe 10/11/2022

TANGAZO LA MARUDIO

1. Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kuitia fedha za Selikari kuu imepanga kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kata ya Nyamwaga.
2. Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anawatangazia mafundi wote wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi za ujenzi waleti maombi kama ifuatavyo:

| | Maelezo ya kazi | Namba ya zabuni |
|---|--|-----------------------------------|
| 1 | Ujenzi wa nyumba ya mtumishi, fence, Kibanda Cha mlinzi nyumba ya Mkurugenzi katika kata ya Nyamwaga | LGA/067/2022-2023/ W/ FA/03 |
| 2 | Ujenzi wa nyumba 1 ya mkuu wa Idara katika Halmashauri ya wilaya ya Tarime kata ya Nyamwaga | LGA/067/2022-2023/ W/ FA/04 LOT 1 |
| 3 | Ujenzi wa nyumba 1 ya mkuu wa Idara katika Halmashauri ya wilaya ya Tarime kata ya Nyamwaga | LGA/067/2022-2023/ W/ FA/04 LOT 2 |
| 4 | Ujenzi wa nyumba 1 ya mkuu wa Idara katika Halmashauri ya wilaya ya Tarime kata ya Nyamwaga | LGA/067/2022-2023/ W/ FA/04 LOT 3 |

SIFA ZA MAFUNDI

- Mwombaji awe Mtanzania
- Mwombaji awe na barua ya utambulisho kutoka kwa mwenyekiti wa mtaa au **Mtendaji wa Kijiji** ikiwa na picha.
- Mwombaji awe na akaunti Benki
- Mwombaji awe na utambulisho wa mlipa kodi (TIN namba)
- Mwombaji awe tayari kukosolewa au kushauriwa na mhandisi wa ujenzi
- Mwombaji asiwe amewahi kushitakiwa kwa kosa lolote la kihalifu au kushindwa kutekeleza kazi zinazofanana na hizi.
- Mwombaji awe na uwezo wa kusoma na kutafasiri michoro na ramani

- Mwombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo ya Serikali
- Fundi atakayefaulu kupata kazi atapewa jaribio la kujenga kwa vitendo.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Nyaraka zote zinapatikana katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ya Zamani (BOMANI) chumba namba 29 Kitengo cha Manunuzi Na Ugavi . kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri Siku za kazi. (Jumatatu hadi Ijumaa).

2. Barua ya maombi na nyaraka zote za zabuni ziwekwe kwenye bahasha na kufungwa vizuri na kuandikwa juu ya bahasha maneno ya fuatayo:-

KATIBU WA BODI YA ZABUNI

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME,

S.L.P 16,

TARIME.

MFANO

Ujenzi wa nyumba ya mtumishi nyumba ya mkurugenzi katika kata ya Nyamwaga ZABUNI NA. LGA/067/2022-2023/ W/ FA/03

3. Mwisho wa kurudisha maombi ni tarehe **18/11/2022** saa **4:00 Asubuhi na baadaye zitafunguliwa saa 4:30 asubuhi.** Maombi/zabuni zitakazochelewa, za kielektroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji wa zabuni kwa hali yoyote ile hazitapokelewa wala hazitakubaliwa kwa tathimini.

Solomon I. Shati

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME**

*DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
TARIME DISTRICT COUNCIL*